**MKATABA**

*KATI YA*

**JOHN BOSCO MVULA,**
**WILLEY LAZARO**
**&**
**DEW LIMITED**

**("Wauzaji")**

*NA*

**LAKE COAL MINING LIMITED**
**("Mnunuzi")**

Mkataba wa Mauziano ya Leseni za Uchimbaji Makaa ya Mawe.

**Umeandaliwa Na:**

JAMES SOSTEN KISINDA
P. O. Box 12630
DAR ES SALAAM

James Kisinda
P.O.Box 12630 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public &
Commissioner for Oaths

**MKATABA WA MAUZIANO YA LESENI YA UCHIMBAJI WA MAKAA YA MAWE**

Mkataba huu umetiwa saini leo tarehe 2, Mwezi wa Tatu, mwaka 2023

**KATI YA**

**JOHN BOSCO MVULA** myenye Sanduku la Posta 1056 SONGEA ,**WILLEY LAZARO** wa Sanduku la Posta 760 SONGEA na **DEW LIMITED** wa Sanduku la Posta 78058 Dar es Salaam (ambao katika Mkataba huu watajulikana kama "**Wauzaji**") kwa upande mmoja.

**NA**

**LAKE COAL MINING LIMITED** mwenye Sanduku la Posta 5055 Dar es Salaam (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "**Mnunuzi**") kwa upande mwingine.

**AMBAPO:-**

Wauzaji ni wamiliki halali wenye leseni ya uchimbaji wa makaa ya mawe yenye namba zifuatazo.

**PML NO (Primary Mining Licence)**

| PML NO | Mmiliki |
|---|---|
| 1. 2330- RVM | **JOHN BOSCO MVULA**<br>**P.O. BOX 1056 - SONGEA** |
| 2. 2331-RVM | |
| 3. 2734-RVM | **WILLEY LAZARO**<br>**P.O. BOX 760 – SONGEA** |
| 4. 2735-RVM | |
| 5. 2794-RVM | |
| 6. 2795-RVM | |
| 7. 2796-RVM | |
| 8. 2797-RVM | |
| 9. 2798-RVM | |
| 10. 2504-RVM | **DEW LIMITED**<br>**P.O. BOX 78058 – DAR ES SALAAM** |
| 11. 2788-RVM | |
| 12. 2789-RVM | |
| 13. 2790-RVM | |
| 14. 2791-RVM | |
| 15. 2792-RVM | |
| 16. 2793-RVM | |

## MKATABA HUU UNASHUHUDIWA NA PANDE ZOTE MBILI KAMA IFUATAVYO

1. Kwamba Wauzaji wanauza leseni za uchimbaji wa makaa ya mawe zilitojwa kwenye ukurasa wa pili wa mkataba huu kwa gharama ya dola za Ki Marekani 280,000 USD yani pesa za Ki Tanzania Shilingi Milioni Mia sita sitini na sita na laki moja elfu ishirini na tu ( Tsh 666,120,000/=) kwa jumla ya leseni kumi na sita, ikiwa ni malipo ya mauziano haya ambayo yatafanyika kwa mkupuo mmoja.
2. Kwamba Wauzaji na Mnunuzi kwa pamoja wamekubaliana kwamba malipo yote kwa ajili ya ya ununuzi wa leseni husika yatafanyika kupitia akaunti ya benki namba **01J2062182802 CRDB BANK PLC** yenye jina **ELIAS LUPITUKO MIGODELA** ambae ni mshirika wa wauzaji.
3. Kwamba baada ya pande zote mbili kuweka sahihi katika mkataba huu, Mnunuzi atawalipa wauzaji gharama za ununuzi wa Leseni husika kama inavyoonyesha katika kipengere cha kwanza kwenye mkataba huu na ushahidi wa ki benki utatumika kuthibitisha malipo kufanyika.
4. Kwamba baada ya malipo kufanyika kwa mujibu wa mkataba huu, wauzaji watafanya mchakato wa kuomba kibali cha Afisa wa Madini ili kukamilisha mabadiliko ya majina kutoka kwa wauzaji kwenda kwa mnunuzi.
5. Kwamba Wauzaji wanathibitisha bila shaka lolote kuwa leseni za uchimbaji wa madini wanazomuuzia mnunuzi ni mali zao na wana miliki leseni hizo kwa mujibu wa sheria.
6. Kwamba Wauzaji wanathibitisha kuwa leseni tajwa ndani ya mkataba huu hazina mgogoro wa aina yoyote, wala zuioa lolote la Ki Sheria, pia hakuna shauri lolote linalohusu leseni hizo kwenye Mahakama yoyote nje na ndani ya Tanzania.

7. Kwamba Wauzaji wanathibitisha kuwa leseni tajwa ndani ya mkataba huu pia hazijawekwa rehani mahali popote au kwa mtu yeyote wala hazijauzwa kwa mtu yeyote isipokuwa Mnunuzi katika mkataba huu.
8. Kwamba baada ya pande zote mbili za mkataba huu kutia sahihi na malipo yote yaliyokubalika na pande zote mbili kufanyika, Mnunuzi ana haki zote za kumiliki leseni hizo na kuzitumia na kuendeleza kadri atakavyotaka kwa mujibu wa mkataba.
9. Kwamba baada ya uthibitisho wa malipo Wauzaji watampatia Mnunuzi vielelezo vyote halisi vya umiliki wa leseni husika.
10. Kwamba gharama za serikali ikiwa kodi mbalimbali zitalipwa na Wauzajikatika mkataba huu baada ya manunuzi kukamilika.
11. Kwamba, Wauzaji wanahaidi ushirikiano wote ambao sio wa kifedha kwa Mnunuzi pale utakapohitajika.
12. Kwamba Mnunuzi anaweza kuendelea na uchimbaji wa madini ya aina yoyote tofauti na Makaa ya Mawe endapo aina hiyo nyengine itapatikana kwenye leseni tajwa hapo juu.
13. Kwamba kwa kutia saini mkataba huu ita maanisha kuwa pande zote mbili katika mkataba huu zimekubaliana na vipengele vyote vya mkataba huu na kuwa tayari kuvitekeleza.
14. Kwamba wafuatao hapa chini watashirikiana na Mnunuzi kuhakikisha Mgodi unaanza kazi.

    I. Bosco Mvule – Mining Blasting
    II. Alfred Machumu- Mining Engineer
    III. Hezron Elias Migodera- Mining Manager
    IV. Elias Lupituko Migodera- Mining Director

## WAHUSIKA HAPA WANAKUBALIANA KUWA:-

Hakuna Mkataba wowote unaoongeza, unaobatilisha, unaofuta au unaoondoa kipengele chochote cha Mkataba huu isipokuwa mpaka Mkataba huo uwe umewekwa kwenye maandishi na kusainiwa na wahusika katika mkataba huu.

Wahusika wamekubali kusaini na kuhakikisha kuwa malengo ya Mkataba huu yanafikiwa.

## USULUHISHI:-

Endapo kutatokea Mgogoro wowote kuhusu mkataba huu utasuluhishwa pamoja kati ya pande mbili husika, ikishindikana, wahusika watapeleka mashauri yao kwenye vyombo vya Sheria.

## MENGINEYO

Jambo lolote litakalotokea ama kuhusisha mkataba huu litakuwa linaongozwa na kutafsiriwa kwa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KAMA USHAHIDI**, Wahusika wameweka saini zao kwenye Makubaliano haya hapa Songea kwa namna na kwa tarehe kama inavyoonekana hapa chini

**Imesainiwa** na **Bosco Mvula** kwa niaba ya **DEW LIMITED** wa sanduku la Posta **78058 Dar es Salaam** leo tarehe 02 Mwezi wa 3 mwaka 2023 katika uwepo wetu.

SIGN HERE

MUUZAJI

**JINA:** JAMES KISINDA

**ANUANI:** S.L.P 12630 DSM

**KAZI/WADHIFA:** AFISA KIAPO

**SAHIHI:** ____________________

James Kisinda
P.O.Box 12630 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public &
Commissioner for Oaths

**Imesainiwa** na **JOHN BOSCO MVULA** leo tarehe 02 mwezi wa 3 Mwaka 2023 mbele ya uwepo wangu.

SIGN HERE

MUUZAJI

**JINA:** JAMES KISINDA

**ANUANI:** S.L.P 12630 DSM

**KAZI/WADHIFA:** AFISA KIAPO

**SAHIHI:** ____________________

James Kisinda
P.O.Box 12630 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public &
Commissioner for Oaths

Imesainiwa na WILLEY LAZARO

leo tarehe 02 mwezi wa 03 Mwaka 2023

mbele ya uwepo wangu.

MUUZAJI

SIGN HERE

JINA: JAMES KISINDA

ANUANI: S.L.P 12630 DSM

KAZI/WADHIFA: AFISA KIAPO

SAHIHI:

James Kisinda
P.O.Box 12630 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public &
Commissioner for Oaths

**Imesainiwa** na **Zakayo Benito Mgaya** kwa niaba ya

**LAKE COAL MINING LIMITED**

wa sanduku la Posta 5055

**Dar es Salaam** leo tarehe 02

Mwezi wa 03 mwaka 2023 katika uwepo wetu.

MNUNUZI

SIGN HERE
ZAKAYO

JINA: JAMES KISINDA

ANUANI: S.L.P. 12630 DSM

KAZI/WADHIFA: AFISA KIAPO

SAHIHI:

James Kisinda
P.O.Box 12630 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public &
Commissioner for Oaths